Si jambo la kawaida mwanadamu kula Udongo!.. Hivyo inapotokea mtu anakula udongo kupitiliza, basi hilo laweza kuwa tatizo la kiroho zaidi ya kuwa tatizo la kisayansi..

Ndio zipo tafiti chache zinazoonesha kuwa mwanamke anapokuwa mja mzito anaweza kuwa na hamu ya kula udongo, na pia mtu aliyepungukiwa na madini Fulani mwilini anaweza kula udongo..

Tafiti hizi zaweza kuwa kweli kwa sehemu, lakini inapotokea Mtu chakula chake kinageuka kuwa udongo, na wengine hata baada ya kumaliza kubeba ujauzito bado wanaendelea kula udongo, na hata kwenda kununua basi hilo ni tatizo la kiroho Zaidi.

Kwasababu maandiko yanasema anayekula mavumbi/udongo ni nyoka tu peke yake.

> *Mwanzo 3:14 “Bwana Mungu akamwambia nyoka, Kwa sababu umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, NA MAVUMBI UTAKULA SIKU ZOTE ZA MAISHA YAKO”*

Hivyo kama unaona unalo tatizo la kula udongo kwa kiwango cha kushindwa kujizuia, basi ipo roho inayokutumikisha katika hilo, kama tu vile roho ya kujichua, hivyo suluhisho kwanza ni kumkaribisha BWANA YESU katika maisha yako, kwa kutubu na kumaanisha kuacha dhambi, kisha kutafuta ubatizo sahihi wa maji mengi na kwa jina la BWANA YESU, na baada ya hapo hiyo roho itaondoka yenyewe na utarudi kuwa mtu wa kawaida.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

TATIZO LA VISIGINO KUUMA KIBIBLIA

JE TATIZO LA KULA KUCHA NI ISHARA YA KUWA NA MAPEPO?

TATIZO LA NDANI LINALOWASUMBUA VIJANA, WALIOOKOKA.

Kunyoa denge ni kufanyaje na je ni dhambi? (Walawi 19:27).

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp